ictj chapisho fupi

ICTJ Justice Truth Dignity

Agatha Ndonga
November 2019

Mabadiliko Katika Sekta Ya Usalama Ya Kenya

Tamaduni za Kazi ya Polisi Na Vijana

Kuibuka kwa mzozo wa kisiasa kufuatia uchaguzi wa urais wa 2017 nchini Kenya, Rais Uhuru Kenyatta na Mheshimiwa Raila Odinga waliamua kujadili makubaliano ya amani. Kwa pamoja, walitoa uwasiliano wa pamoja wenye jina "Building Bridges to a New Kenyan Nation," ambapo walitangaza mpango wa "kuunda taifa moja kwa Wakenya wote wanaoishi sasa, na vizazi vyote vijavyo" na kuafikia malengo yao ya pamoja ya masuala tisa muhimu.[1] Mpango huo unaoongozwa na kikosi cha Wajumbe 14 kwa Kiingereza 'Building Bridges to Unity Advisory Taskforce' wanamshauri Rais Kenyatta na Mheshimiwa Odinga kuhusu utekelezaji wa sera zilizokusudiwa kuwezesha suluhisho endelevu nchini Kenya.

Kikosi hiki cha wajumbe kinaagizwa kufanya mashauriano na raia pamoja na vijana, wawakilishi wa sekta ya Imani au dini, viongozi wa kitamaduni, wawakilishi wa sekta ya kibinafsi, na wataalam katika ngazi za kaunti na kitaifa.[2] Mashauriano haya yamekusudiwa kutoa wigo mpana wa jamii ya Kenya nafasi ya kushiriki kwa maana katika Mpango wa Building Bridges Initiative, kupendekeza suluhisho la wasiwasi wao mkubwa, na kusaidia kuunda chombo cha sera.

Walakini, kulingana na vijana ambao waliongea na ICTJ, kikosi hiki cha ushauri kimefanya juhudi kidogo kufikia na kuwashirikisha vijana kutoka makaazi ya vijiji duni vilivyomo mijini kuhusu mada mbali mbali zinazowahusu, haswa marekebisho ya sekta ya usalama. Malalamiko makubwa zaidi yaliyotolewa na vijana kuhusu uzoefu na kukumbana kwao na polisi, hadi sasa yanabakia kuwa matumizi ya nguvu zaidi ya inavyofaa na polisi na haswa katika makaazi yasiyokuwa rasmi au vijiji duni. Vijana hao walisema kwamba matumizi ya silaha kali katika visa vingi visivyoweza kuelezewa unaonyesha sera isiyo rasmi ya mauaji ya jinai. Wale kutoka mitaa ya mabanda walitoa mifano ya kibinafsi ya marafiki na wenzao waliouawa na maafisa wa polisi.[3] Maoni ya hawa vijana juu ya matumizi ya lazima yasiyofaa na ya nguvu kupindukia yanawashirishwa pia na washiriki wa umma.

MEZA YA YALIYOMO

Mtazamo Wa Vijana Kuhusu Mchakato Wa Mazungumzo Ya Kitaifa 4

Adhabu Ya Pamoja 5

Vijana, Ufisadi, Na Polisi 6

Usajiri Katika Sekta Ya Usalama Na Uzoefu Wa Vijana 8

Uhuru Wa Ushirika Na Uzoefu Wa Vijana 8

Mapendekezo Dhidi Ya Sera za Polisi Katika Vikao Vya Mazungumzo Na Vijana 9

Hitimisho 10

1 The issues are (1) ethnic antagonism and competition, (2) lack of a national ethos, (3) inclusivity, (4) devolution, (5) divisive elections, (6) safety and security, (7) corruption, (8) shared prosperity, and (9) responsibilities and rights. www.president.go.ke/2018/03/09/building-bridges-to-a-new-kenyan-nation/.

2 *The Kenya Gazette*, Vol. CXX, No. 64, p. 1658 (Gazette Notice No. 5154).

3 See AkelloOdenyo, "Slums Fear and Revere 'Killer Police Squads,'" *The Star*, February 15, 2019, www.the-star.co.ke/news/big-read/2019-02-15-slums-fear-and-revere-killer-police-squads/. See also "Why Officer Filmed Killing Teenager Is 'Loved' in Eastleigh," *Nairobi News*, April 9, 2017, https://nairobinews.nation.co.ke/news/officer-filmed-killing-teenager.

Tukio moja ambalo bado halijafutika akilini mwa vijana wengi katika makaazi yasiyo rasmi linasisitiza hali yao ya wasiwasi. Mnamo Machi 31, 2017, clipu ya video iliyoonesha kuuawa kwa kijana katika eneo la Nairobi, Eastleigh na afisa wa polisi anayeaminika kuhusishwa na Kituo cha Polisi cha Pangani, Nairobi ilienezwa katika mitandao ya kijamii.[4] Kwenye klipu hiyo, afisa wa polisi aliyevaa mavazi ya raia huonekana akimpiga risasi kijana ambaye alikuwa amejisalimisha na alikuwa amelala chini. Afisa (aliyetambuliwa kama Kopro Ahmed Rashid) alionekana kwa hiari kumuua kijana huyo kinyama.[5] Tukio hili lilitokea karibu na makazi yasiyo rasmi huko Nairobi, mbele ya maafisa wa polisi. Katika hiyo video, wanaweza kuonekana wakiliziba eneo hilo na kuweka watazamaji waliovutiwa kando. Tawi kuu la serikali, kupitia katibu mkuu, lilitetea kitendo hiki cha kukiuka sheria na Huduma ya Kitaifa ya Polisi (NPS), ikishikilia ya kwambwa ni muhimu kupigana na uhalifu.[6]

Tukio hilo linaangazia tena uzoefu wa kikoloni katika sera za kazi ya polisi walizoziunda ili kuwasaidia wanasiasa wakuu wa Uingereza kuwatawala WaAfrika kwa nguvu za kikatili na vurugu kubwa.[7] Mbinu za polisi za awali zilikuwa na mapendeleo makubwa ya ubaguzi wa rangi na matabaka, kutokana na mahitaji ya walowezi kulindwa kisheria sio na watu asili bali na Wazungu wengine. Hali kadhalika, tofauti na maeneo ya walowezi, maeneo ya asili yalilindwa na polisi kwa kiasi 'chembamba' mno. Shughuli kubwa za ulinzi wa polisi kawaida zilishungulikia maeneo ambayo serikali za kikoloni zilikuwa na nia ya kulinda maisha ya walowezi wa Ulaya, mali, maslahi ya kiuchumi, na miundombinu. Ukosefu wa polisi na matakwa ya eneo lililopanuka kulisababisha hali zisizo za kawaida na wakati mwingine aina za utelezaji wa sheria zilizohusisha kuteswa, kuwekwa kizuizini kwa njia haramu, na kunyimwa chakula na mahitaji ya kimsingi wakati wakiwa kizuizini.[8] Mauaji ya huko Eastleigh yanaangazia mtazamo wa jumla — mtazamo ulioigwa na polisi na umma — kwamba madhumuni ya polisi ni kuwalinda matajiri na wakuu kutokana na uhalifu unaofanywa na maskini. Tofauti kabisa na kisa hicho cha Eastleigh ni kile kilichoangaziwa kwenye habari mnamo Oktoba 2018 ambapo afisa wa polisi alisambaratisha tukio la wizi katika eneo la kifahari jijini Nairobi, eneo la Westlands. Katika tukio hili, mwanamume wa asili ya KiAsia na mwengine wa Kiafrika walikamatwa na kushtakiwa Mahakamani, na huyo afisa wa polisi, Joash Ombati, alitambuliwa sio kwa sababu ya kuwazuia wanyang'anyi hao tu, bali pia kupuuza wito wa umma kuwaangamiza watuhumiwa hao mara moja.[9]

Kati ya Aprili 15 na Mei 3, 2019, ICTJ ilifanya mashauriano kadhaa na vijana kutoka makaazi kadhaa duni huko Nairobi na Mombasa kutafakari kuhusu kuelewa kwao juu

4 Abdi Latif Dahir and Lily Kuo, "Kenyan Police Reportedly Killed Two Teenagers in Broad Daylight—and Much of the Public Approved," *Quartz Africa*, April 4, 2017, http://bit.ly/2DtOCZ8.

5 *BBC News Africa*, "Hunting Down Gangsters with Kenya's Ahmed Rashid—Full Documentary—BBC Africa Eye," YouTube, September 9, 2018, www.youtube.com/watch?v=pOjYnSAAcnQ.

6 Medika Medi, Kenya Human Rights Commission, "Police Brutality and Evasive Justice," January 14, 2019, www.khrc.or.ke/2015-03-04-10-37-01/blog/672-police-brutality-evasive-justice.html; Ndung'u Wainaina, "Uhuru's Carte Blanche to Police Driving Kenya into Lawlessness," *Kenya Free Press*, November 18, 2007, www.kenyafreepress.com/top-stories/national/2934/uhuru-s-carte-blanche-to-police-driving-kenya-into-lawlessness

7 Peter Karari, "Modus Operandi of Oppressing the 'Savages': The Kenyan British Colonial Experience," *Peace and Conflict StudiesJournal* 25.1 (2018): Article 2; Truth, Justice and Reconciliation Commission Kenya, "Report of the Truth, Justice and Reconciliation Commission, Volume 2A" (2013), 99, https://digitalcommons.law.seattleu.edu/tjrc-core/.

8 Truth, Justice and Reconciliation Commission Kenya, "Report of the Truth, Justice and Reconciliation Commission, Volume 2A" (2013), 49.; Peter Karari, "Modus Operandi of Oppressing the 'Savages': The Kenyan British Colonial Experience," *Peace and Conflict StudiesJournal* 25.1 (2018):

9 Global Village-Africa, "Joash Ombati, Kenya Police Constable Who Saved a Life and Recovered KSh 400,000 from Armed Robbers," YouTube, October 18, 2018, www.youtube.com/watch?v=TxqNoZWRccU. See also Stella Cherono, "I Was Only Doing My Job, Says Officer in Nairobi Abduction Drama," *Daily Nation*, October 19, 2018, www.nation.co.ke/news/Officer-in-city-abduction-drama/1056-4812612-123eg52/index.html

ya marekebisho ya sekta ya usalama na uhusiano wao katika mchakato wa mazungumzo ya kitaifa unaoendelea, haswa kama yanahusiana na ujumuishwaji. Makaazi haya duni yalichaguliwa kwa sababu yalikuwa yameathiriwa sana wakati wa vurugu za uchaguzi wa 2007 na 2017, na ukiukwaji kadhaa ulioripotiwa katika kila eneo. ICTJ ilitumia nakala yake ya hivi karibuni kuhusu marekebisho ya sekta ya usalama na ujumuishwaji kuongoza mchakato wa mazungumzo haya.[10] Karibu vijana 120, kutoka Dandora, Kayole, na Mukuru Kwa Njenga jijini Nairobi na Changamwe huko Mombasa, walishiriki katika majadiliano haya; kati ya vijana 30 na 40 walishiriki katika kila mjadala. Mchango wao wa mafundisho ulitumika kama msingi wa nakala hii na unapaswa kuunda sehemu muhimu ya mchakato wa majadiliano ya kitaifa kuhusu uhusiano na ujumuishwaji na usalama wa vijana.

ICTJ ilishirikiana na vijana hawa kupitia kikundi kinachojulikana kwa Kiingereza kama Social Justice Centre Working Group na haswa kile cha Dandora, Kayole, Mukuru Kwa Njenga, na Changamwe. Uundwaji wa vituo hivi vya haki za kijamii ni matokeo ya moja kwa moja ya mauaji ya kiholela ya polisi yaliyoshuhudiwa katika maeneo ya mitaa ya mabanda. Vituo hivi vilianzishwa ili kudai uwajibikaji kwa mauaji haya ya vijana kati ya miaka 13 na 24 na kukatalia mbali hali ya kukubalika kwa mauaji haya, na kutafuta suluhu ya ukosefu wa haki za kijamii na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu ambao umetokea zaidi katika mitaa ya mabanda na pia katika vijiji maskini.

Masuala makuu matano (5) yaliyoibuka kutoka kwa vikao hivi vya mazungumzo:

1. Uwekaji wa sera za ulinzi wa polisi nchini Kenya bado umejikita katika kulinda matajiri na wakuu wa kisiasa dhidi ya maskini. Huu ni kwa kuzingatia msingi wa dhana kuwa maskini kwa kawaida ni wahalifu ambao wanapaswa kuzuiwa kuwa kero kwa matajiri na wakuu wa kisiasa.

2. Vijana wanapoona ugandamizaji huu usio na usawa ki sheria, hadhi yao na uraia wao unapuuzwa.

3. Ubaguzi katika uwekaji sera za ulinzi wa polisi umezamisha vijana katika umaskini. Vijana huamua kuwapa hongo polisi ili waweze kurejeshewa uhuru wao wakati wanapozuiliwa bila hatia na kwa nia ya kuzuia kushtakiwa. Vijana wengi walisema kwamba kujaribu kupingana na mashtaka hayo kunamaanisha kuwa watafikishwa katika kituo cha polisi, ambapo watakabiliwa na adhabu kali zaidi, kama vile malipo ya dhamana ya pesa (ambazo wakati mwingi hazifikii hazina ya umma) au faini ya korti au mahakama.

4. Vijana wengi wanaokinzana na sheria wanakosa ushauri wa kisheria au uwakilishi, na kwa hivyo kawaida wanakiri makosa ili kuzuia kuzuiliwa kwa muda mrefu. Matokeo yake, wao hupata rekodi ya uhalifu, ambayo huathiri fursa zao za kupata riziki zenye maana na endelevu katika sekta rasmi ambayo inahitaji vyeti vya polisi vinavyojulikana kama “Good conduct.”

Kuwa kijanana maskini nchini Kenya ni hatia — kama vile adha inavyokwenda katika makazi yasiyokuwa rasmi. Utekelezaji mwingi wa mauaji ya jinai uliofanywa na polisi ni dhidi

10 Christopher Gitari, International Center for Transitional Justice, “Situating Security Sector Reforms in Kenya’s Discourse on Inclusion and National Dialogue Process” (March 2019), www.ictj.org/sites/default/files/ICTJ_Briefing_KenyaInclusionDiscourse_Web.pdf

ya vijana.[11] Uzoefu unaonyesha ya kwamba wakati vijana wanakamatwa na wanashindwa kutoa hongo ili kuachiliwa, wako katika hatari ya kudhulumiwa zaidi kimashtaka.

Mtazamo Wa Vijana Kuhusu Mchakato Wa Mazungumzo Ya Kitaifa

Mauaji Ya Jinai

Zaidi ya miaka sita iliyopita, Tume ya Ukweli, Haki na Maridhiano (TJRC) iliripoti ya kwamba mashirika ya usalama ya serikali, haswa polisi na wanajeshi, kama wahusika wakuu katika kutoa uhai kiholela na ukiukwaji wa haki za binadamu nchini Kenya, ikiwemo mauaji ya halaiki za watu, kutekeleza kutoweka kwa watu kwa lazma, ugandamizaji na unyanyasaji, na dhuluma za kijinsia.[12] Tume ya Kitaifa ya Kenya ya Haki za binadamu (KNCHR) imewashilisha ripoti mbili — "The Cry of Blood" mnamo Septemba 2008 na "The Error of Fighting Terror with Terror" mnamo Septemba 2015 — ambalo lililenga mauaji ya jinai na kutowesha watu kwa lazma.[13] Ripoti ya kwanza ilisisitiza matokeo ya hapo awali ya hilo tume: Kati ya Juni na Oktoba 2007, polisi walikuwa wamewaua watu 500 wengi wao wakiwa vijana walioshukiwa kuwa washiriki wa Mungiki, genge la uhalifu lililotokana na jamii ya Wakikuyu. Katika ripoti ya pili, KNCHR ilipata kuwa katika Nairobi na sehemu za pwani na kaskazini mashariki, polisi na wanajeshi walihusika kwa pamoja kuangamiza na kutoa uhai au kutowesha watu wapatao 120 kwa kipindi cha mwaka mmoja kilichorekodiwa mnamo mwaka wa 2015. Waathiriwa walikuwa vijana wa kiume walioshukiwa kuwa wanachama wa kikundi cha kigaidi cha Al Shabaab. Akithibitisha matokeo haya, kijana ambaye alishiriki katika mazungumzo ya 2019 na ICTJ aliwataja wenzi wengine ambao aidha waliangamizwa na polisi au kutoweka baada ya kuchukuliwa na maafisa wa polisi.

Kulingana na Shirika la Independent Medico-Legal Unit (IMLU), kipindi cha 2014 hadi 2017 kiliona mwenendo wa polisi wa kutumia silaha kihatari, ikiwa ukiukaji wa Sheria ya NPS (NPS Act). IMLU iliripoti ya kwamba mnamo mwaka wa 2014 kulikuwa na visa 34 vilivyoripotiwa vya mauaji ya ghafla, na katika mwaka wa 2015 kulikuwa na visa 27; kisha, kulikuwa na kuongezeka maradufu katika utumiaji wa nguvu mnamo 2016, na hati 122 zilizorekodiwa za mauaji ya ghafla.[14] Hakuna maelezo ya kutosha ambayo yametolewa kwa matumizi haya ya nguvu zaidi, na NPS haijachunguza vifo hivi kama inavyotakiwa na Sheria ya NPS (NPS Act).

Ubaguzi Unaotekelezwa na Polisi

Kwa sababu ya kiwango cha juu cha ukosefu wa ajira kwa vijana nchini Kenya (kwa asilimia 42 mnamo 2017), idadi kubwa ya vijana ni maskini.[15] Kulingana na UNICEF, asilimia 62 ya idadi ya watu nchini Kenya ni chini ya miaka 24, na zaidi ya asilimia 75 ya watoto na vijana wameshuhudia au kunyimwa moja au zaidi ya haki zao za kiuchumi

11 Independent Medico-Legal Unit, "Deaths from Police Bullets from January to December 2016: Report on Extrajudicial Executions by State Agents in Kenya" (2016), https://imlu.org/index.php/shortcode/reports/typgraphy/send/3-reports/46-extra-judicial-executions-2016-full-report.

12 TJRC Kenya, "Report" (2013), 33.

13 KNCHR, "The Cry of Blood: Report on Extra-Judicial Killings and Disappearances" (2008); KNCHR, "The Error of Fighting Terror with Terror: Preliminary Report of KNCHR Investigations on Human Rights Abuses in the Ongoing Crackdown against Terrorism" (September 2015).

14 Independent Medico-Legal Unit, "Deaths from Police Bullets Reports" (2014-2017). See: https://imlu.org/index.php/shortcode/press-release; https://imlu.org/index.php/shortcode/reports/typgraphy?start=20; https://imlu.org/index.php/shortcode/reports/typgraphy/send/3-reports/46-extra-judicial-executions-2016-full-report

15 Samuel Hall, UK Department for International Development, "Youth Employment in Kenya" (October 2017), www.britishcouncil.co.ke/sites/default/files/ng_kenya_youth_employment_in_kenya.pdf.

na kijamii.[16] Umaskini huu huwafanya wawe katika hatari ya kunyanyaswa zaidi. Vituo vyote vya haki vya kijamii (social justice centres) ambavyo vilihushisha ICTJ vinasema kwamba maafisa wa polisi wameharamisha umaskini kwa kulenga vijana kwenye mitaa ya mabanda, huku wakidai hongo, mauaji ya ghafla, na kutoweshwa. Vijana kutoka maeneo haya wanalinganisha mwenendo wa polisi kwao kwa jumla na katika maeneo tajiri ya Kenya na Nairobi haswa, ambapo vijana hawasumbuliwi, hawafungwi kinyume na sheria, kudaiwa hongo, kuteswa, au kuuliwa kikatili na polisi. Hii, wanaamini, ni kwa sababu maskini kawaida hufikiriwa kuwa wahalifu, tofauti na wale walio katika maeneo ya kifahali. Kulingana na washiriki katika majadiliano hayo, licha ya kufanya mafunzo, polisi wanajizuia katika maeneo yamatajiri lakini hawatasita kupiga risasi vijana huko Dandora, Mathare, au Kayole bila au kwa sababu zisizo na msingi badala ya kuwafikisha mahakamani ikiwa wamehusika na uhalifu. Kwenye maeneo ya mabanda, maafisa wa polisi hawawapi nafasi vijana kujieleza au kueleza vitendo vyao, kama jinsi wangewapa wenzao katika maeneo tajiri zaidi. Kwa hivyo, mapendekezo kwamba wakaazi wa mitaa ya mabanda wanapaswa kujibeba kiheshima (hiyo ni kama “mtu tajiri”) ni mbaya. Katika mkoa wa pwani na kaskazini mashariki, polisi wanawahushisha vijana wa kiislamu na ugaidi, huku vijana wengi wakiuliwa, wakitoweshwa baada ya kukamatwa kiholela au kutuhumiwa kwa makosa ya ugaidi.

Ubaguzi wa ukiukaji sera za ulinzi wa polisi unaongeza zaidi kutengwa ambako kulianzishwa na wakoloni na ambao umeendelea kwa miongo kadhaa.[17] Miundo ya kiuchumi, kijamii, na kutengwa kisiasa kulianzishwa na wakoloni wa Uingereza na kukuzwa na serikali zilizofuata za uhuru zimesababisha umbo la umaskini na ukosefu wa usawa katika kupeana huduma muhimu.[18] Kulingana na vijana waliochangia kwenye mazungumzo, wale ambao wanajihusisha na uhalifu hufanya hivyo kutokana na umaskini uliokithiri na unaoonyesha hali ya maisha yao ya kila siku. Dhuluma za kimuundo zinazowakabili zinaweza kulaumiwa tu kwa serikali, ambayo haifanyi chochote kutoa nafsi za kazi zinazohitajika sana na kwa hivyo inawanyima fursa ya kujipatia riziki nzuri. Hakungekuwa na ukosefu wa usalama ikiwa vijana wangekuwa na kazi. Kama mshiriki mmoja alivyosema kwa muhtasari, “Usalama ni shibe kamili. Mtu hajihusishi na uhalifu ikiwa amelishwa vizuri au ameshiba.”

Kulingana na vijana walioshiriki, NPS inapaswa kujifunza au kuomba kutoka kwa sehemu au nchi ambazo wafungwa wa zamani hukubaliwa tena na jamii baada ya kutumikia kifungo chao, na ambapo wanapewa nafasi ya kujiunga na sekta ya usalama. Hapa Kenya, vijana waliorekebishwa kwa dhati bado wanalengwa katika kudhulumiwa, ambayo ni bure kwa sababu inawapelekea baadhi yao kurudi kwenye uhalifu. Kutofuta rekodi za jinai za vijana waliobadilika baada ya kipindi fulani huongeza tu ubaguzi, pamoja na kuzuia vijana kupata ajira katika siku za baadaye.

Adhabu Ya Pamoja

Mawakala wa usalama bado hutekeleza adhabu ya pamoja, wakiwalenga zaidi vijana katika mitaa ya mabanda. Adhabu ya pamoja kama hiyo kawaida hutumika na jamii wakati wa maandamano ya kisiasa au wakati wowote kikundi kisichojulikana cha watu au genge kinapokiuka sheria. Sekta ya usalama inachukulia hatua za kulipiza kisasi kwa jamii kwa jumla na kwa njia ya vurugu, kama njia ya kutuma ujumbe kwa genge au kuadhibu jamii kwa tuhuma za “kuficha” hao wahalifu. Vijana waliolishiriki katika majadiliano

16 UNICEF, “Kenya at a Glance: Situation of Children and Adolescents,” www.unicef.org/kenya/overview_15603.html.
17 TJRC Kenya, “Report” (2013), 20.
18 Gitari, “Situating Security Sector Reforms.”

walielezea kuwa majibu ya polisi katika matukio hayo hufuatiwa na kukamatwa kwa vijana wengi kwa pamoja, kudaiwa hongo na kutiwa kizuizini pasipo uhalali. Katika visa vingine, vijana wanapinga kukamatwa au kujitetea dhidi ya unyanyasaji na afisa wa polisi, lakini baada ya hapo vijana na wanaume kutoka eneo hilo hukusanywa na kuadhibiwa kwa pamoja kupitia mateso na kupigwa. Polisi huonekana mara nyingi kupuuza ukweli kwamba wakati mtu mmoja au wawili hufanya kosa, haimaanishi kwamba jamii nzima ina hatia.

Adhabu ya pamoja ilionekana wakati wa uchaguzi mkuu wa 2017 na KNCHR. Katika ripoti yake ya 2017, KNCHR ilibaini kuwa polisi wangeungana pamoja na kuwatia nguvuni vijana katika mitaa ya mabanda ya mijini wakati wa shughuli za polisi.[19] Ilirekodi kesi za udhalilishaji, kushambulia, na kukamatwa kiholela kwa wakaazi kufuatia kupelekwa kwa maafisa wa polisi jijini Nairobi (haswa katika Dandora Awamu ya 4), kule Kisumu (huko Nyalenda, Ahero, na Awasi), na huko Mombasa (Bokole na Changamwe) — wengi wa hawa waliokamatwa wakiwa katika makazi yasiyokuwa rasmi. Waathirika wengi walikuwa wa kiume na walikusanywa kwa pamoja na polisi. Katika visa vingi vilivyoandikishwa, maafisa wa polisi waliingia kwa nguvu katika nyumba za watu, wakitafuta vijana ambao baadaye walikamatwa na kuwekwa kizuizini kwa muda mrefu.[20]

Ripoti ya TJRC inabainisha kuwa ukiukaji sera za utekelezaji wa kazi ya polisi nchini Kenya kutoka zamani wameonyesha utayari fulani wa kuepuka na kupuuza sheria chini za kufanya kazi katika mazingira magumu. Hii ilionyeshwa vyema kila wakati eneo asili lilipoelezewa kama “lililosumbuliwaa au hatari;” kwa kuongezea, jamii zinazokaa katika eneo hilo pia zingeitwa hatari na tishio kwa usalama wa taifa. Sherehe maalum ziliwekwa chini ya Sheria ya Adhabu ya Pamoja (Collective Punishment Ordinance), ambayo iliruhusu jamii nzima kuadhibiwa kwa makosa ya wachache. Polisi wangedai malipo hayo kutoka kwa jamii kwa gharama ya operesheni iliyozinduliwa ili kuzirekebisha na kujitosheleza. Kwa hivyo, polisi basi wangevamia mali ya jamii huku wakidai ni kufuata sera za utekelezaji wa kazi ya polisi.

Chini ya operesheni zote ilihisiwa kwamba watu walipaswa kuadhibiwa, kugandamizwa na ikiwa ni muhimu— walilazimishwa kuelewa kwamba walipaswa kufuata sheria za kibaguzi na kanuni zilizotumika wakati wa ukoloni. Ubatili wa kutumia njia kama hizo za kukandamiza ili kutekeleza heshima kwa sheria haukueleweka kabisa na wanamamlaka.[21]

Vijana walioshiriki kwa mazungumzo wanahisi kwamba NPS inapaswa kufikiria tena jinsi inavyofanya shughuli za kuwapeleka polisi kwa vituo. Polisi wanapaswa kupelekwa kwa vituo ambako watawatumikia jamii zao kwa faida ya ufanisi na kinga dhidi ya dhuluma, kwani hawawezi kukiuka haki za mwananchi wa jamii yao na kwa sababu wanajua eneo na nguvu za eneo hizo. Kupelekwa kwa maeneo ambayo hayajulikani kunaonekana kama hatua ya makusudi ya kufanya operesheni ambazo wakati mwingine husababisha ukiukwaji.

Vijana, Ufisadi, Na Polisi

Vijana huchukulia idara ya polisi kuwa taasisi ya ufisadi kutoka kileleni hadi chini. Ukiukaji wa haki za binadamu unaofanywa na polisi mara nyingi hufanyika wakati wahasiriwa wanakataa kutoa hongo au kugandamizwa kifedha. Maafisa wa polisi pia wanahusika vikubwa katika kupinga haki wakati wanachukua hongo kuzuia uchunguzi. Kijana mmoja alitoa mfano wa msichana wa Kisomali ambaye alibakwa na mhalifu

19 KNCHR, “Mirage at Dusk: A Human Rights Account of the 2017 General Elections” (2017).
20 Ibid., 211.
21 TJRC Kenya, “Report” (2013), 59.

tajiri, ambaye hapo hapo aliwapatia polisi hongo kusambaratisha hiyo kesi kortini. Polisi pia wanaonekana kuwa wanatumiwa na serikali kulinda maafisa wafisadi. Wakati jamii zinaungana kuandamana dhidi ya unyonyaji au uporaji wa aina yoyote, kama matumizi mabaya ya fedha za umma, unyakuzi wa ardhi, kufungwa kwa barabara za umma, au mifereji ya maji taka, kwa mfano, serikali mara nyingi hujibu kwa kutuma maafisa usalama (ambao wakaazi wa makaazi duni hutaja kama "red Beret") ambao hawashirikiani na waandamanaji ili kujua na kushughulikia sababu za maandamano, lakini badala yake wanawapiga raia na wakati mwingine huwaumiza au kuwaua.

ICTJ ilipata yafuatayo katika sera yake ya kifupi juu ya zoezi la kuwachuja polisi nakufichua mitandao ya ufisadi katika NPS:

> Wakati wa mchakato wa mchujo, maafisa kadhaa wa trafiki wa vyeo vya chini walikiri kutuma mali zilizopatikana kinyume na sheria (hongo) kwa wakubwa wao kwa muda mrefu kwa njia ya simu za mkononi au rununu — na hawakuweza kuelezea ukweli wa vyanzo vya mali zao au sababu za kuendelea kutuma pesa kwa wakubwa wao. Hii ilikiingiza kikundi cha maafisa waandamizi wa polisi katika makosa, ambao baadhi yao walikuwa wamepatikana bila hatia na NPSC [Tume ya Kitaifa ya Huduma ya Polisi] wakati wa mchakato wa kuchuja. NPSC ilikuwa na ugumu kuelezea kutofaulu kwake kuondoa maafisa wakuu waandamizi waliopatikana bila hatia.[22]

Kulingana na ripoti ya Transparency International, wafanyikazi wengi katika sekta ya usafiri wa umma walipendelea kutoa hongo kwa polisi wanapokamatwa kwa kuvunja sheria za trafiki. Asilimia 80 ya madereva wa treila na waendeshaji bodaboda walikubali kwa urahisi kulipa hongo maafisa wa polisi, wakisema kwamba mfumo wa mahakama hauaminiki katika kukabiliana nao ipasavyo. Polisi, maafisa wa mashtaka, na maafisa wa mahakama pia wanatumia vibaya mamlaka yao kuhakikisha kwamba wale wanaotumia mfumo wa haki wanagandamizwa sana na kulipa faini kubwa wanapopatikana na hatia.[23]

Vijana walioshiriki walidokeza kwamba ikiwa Kenya itakuwa nchi ya kidemokrasia zaidi, lazima ijitahidi kumaliza ufisadi ambao umekita mizizi kwenye sekta ya haki, ambayo inautengaji kwa kupendelea wale ambao wanaweza kutoa hongo na kushutumu wale ambao ni masikini na hawawezi kutoa hongo. Vijana walioshiriki walisema kwamba wanakabiliwa na kuzuiliwa kwa muda mrefu na vifungo vya gereza kwa sababu hii hii. Vijana wengi pia hawana uwezo wa kuajiri mawakili na hivyo basi wanakiri mashtaka ambayo wanaweza kuwa na utetezi halali. Vijana wanahisi kwamba mahakama katika ngazi ya serikali za kaunti inapaswa kushughulikia makosa madogo, kama vile kutafuta wasafiri kimabavu, kuzurura ovyo na kuchuuza, ambazo polisi wametumia kudai hongo. Hivi sasa, wale wanaofanya makosa kama hayo hufungwa pamoja na wauaji na wezi wa kimabavu; vijana walioathirika huishia kutumikia vifungo gerezani wakati wanaposhindwa kutoa hongo au dhamana. Sheria zinazoruhusu kukamatwa kiholela na madai ya kutishia kama vile uvivu, ulevi na usumbufu, na kuzurura ovyo zinapaswa kuondolewa. Sheria hizi zimetumiwa na polisi kuwadhulumu vijana, huku maafisa hata huweka "ushahidi" bandia juu yao ili kuwashtaki kwa uhalifu.[24]

22 Hilton Otenyo, "Traffic Bosses Extort Money from Juniors, Vetters Learn," The Star, August 18, 2016, www.the-star.co.ke/news/2016/08/18/traffic-bosses-extort-money-from-juniors-vetters-learn_c1405042; K24 TV, "Vetting Reveals How Senior Police Officer Demand Money from Juniors," *YouTube*, May 25, 2016, www.youtube.com/watch?v=oeejtQVovhU

23 Transparency International, "Traffic Legislation Gaps and Drivers of Corruption in Traffic Matters" (2018), 17.

24 Young people gave examples of officers forcing youth to carry machetes or pangas and taking photos of them, and thereafter framing them as part of a ferocious criminal gang in Mombasa known as Wakali Kwanza

Usajiri Katika Sekta Ya Usalama Na Uzoefu Wa Vijana

Vijana kadhaa walioshiriki walisema ya kwamba wameshiriki katika mchakato wa kuajiriwa kujiunga na NPS au Kikosi cha Ulinzi cha Kenya (KDF). Waajiri wengi, badala ya kutoa uamuzi wakimsingi kulingana na uhitimu wa waombaji usajiri, walidai hongo au kuwatenga waombaji ajira au kuwatenda kwa misingi ya kikabila. Machoni mwa vijana wengi, mazoezi ya kusajiri yanafanywa kwa madhumuni ya uhusiano wa umma tu kwani waajiri tayari wameshatumia tasnia-haswa kupitia mapendeleo au hongo. Kutengwa kwa misingi ya kijinsia pia huendelezwa wakati wa kuajiri; wanawake hupata nafasi chache ingawa wanakabiliwa na viwango tofauti na wakati mwingine viwango vilivyorahisishwa katika mazoezi ya kusajiri. Jukumu la utoaji wa hongo ili kusajiri katika NPS na KDF inalaumiwa kwa kuongezeka kwa ufisadi katika sekta ya usalama na kutojitolea kwa dhati kwa maafisa wa kutumikia umma na kulinda sheria. Katika uamuzi wa Mahakama Kuu, korti ilikubaliana na Tume ya National Police Service Commission iliyogundua kwamba zoezi la kuwachukua polisi la mwaka 2014 lilikuwa limejawa na mapendeleo, ufisadi, ukabila, na mienendo mingine mibaya.[25] Ingawa tume hiyo ilisema kwamba dosari hizo hazijaenea, korti haikukubaliana na ikagundua kuwa zoezi hilo lilistahili kufutiliwa mbali kwa jumla. Masuala ya vijana kwa hivyo yamedhibitiswa haki: Njia ambazo polisi wa kusajiri maafisa bado zina dosari na kwa kweli zinachangia hisia za kutengwa.

Vigezo vingine vinavyohusiana na usajiri kwa polisi ambazo vijana waliona kuwa hutumiwa kuwatenga kwa kimo fulani, kuwa na urefu fulani, kuwa na idadi kamili ya meno, na kukimbia kwa kasi fulani, badala ya kwa ujumla kuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu yanayotarajiwa. Viwango hivi pia vinachangia kwa kutoelewa kwa mahitaji ya kazi katika huduma ya polisi (yaani, kutumikia umma na kutunza sheria na utaratibu). Ingawa maoni ya vijana ni halali, kuna sababu halali za kuwekwa kwa vigezo vinavyohusiana na maumbile, kwa kuzingatia asili ya kazi hiyo, eneo la kufanya kazi, na madai ya kimwili ya sera za kazi ya polisi za ulinzi; kigezo cha muhimu ni jinsi vinavyofikiwa na kutumika.

Uhuru Wa Ushirika Na Uzoefu Wa Vijana

Kunaendelea kuongezeka, jamii na haswa zenye uwakilishi mdogo ambazo sauti zao zimepuuzwa hapo zamani zinagundua kuwa maandamano ni nyenzo muhimu ya kusiikilizwa. Wanakerwa na ukosefu wa hatua ambayo inafuatia mazungumzo na wakuu wa serikali na wanaamua kufanya maandamano ya kupigania kutengwa — kwa mfano, kupinga udhalilishaji na maafisa wa polisi na wakuu wa polisi na wasaidizi wao, au kudai kuboreshwa kwa miundomsingi, kama mabomba ya maji na barabara, na dawa katika zahanati za mitaa. Pia wanageukia korti wakati inapostahili. Kwa maandamano kufaulu, jamii lazima zijue haki zao na jinsi ya kuelezea mahitaji yao, ambayo yanahitaji kuendelea kuhamasishwa. Majibu ya serikali kwa maandamano mara nyingi huwa ya vurugu, ingawa haya majibu inaripotiwa kuwa inalingana na eneo la maandamano. Katika miji mikubwa, mitaa ya mabanda kama Kibera, na mkoa wa magharibi, kukabiliana na hali hiyo huhusisha matumizi ya vitoa machozi na zana nyingine za kupambana na ghasia, ingawa katika maeneo mengine, kama mkoa wa kaskazini mashariki, watu wameuawa. Majibu yasiyo ya fujo kwa maandamano mara nyingi hujumuisha suluhisho la haraka, na la muda mfupi-kwa mfano, kujibu maandamano kuhusu uhaba wa maji kwa kutoa tanka za maji, badala ya kutoa suluhisho la kudumu kama vile kuwekewa bomba na mifereji ya maji na pamoja na yale ya maji taka.

25 *Independent Policing Oversight Authority and another v Attorney General and 660 others*, Petition 390 of 2014; see http://kenyalaw.org/caselaw/cases/view/103031/.

Maafisa wa polisi wanapaswa kuheshimu maandamano, ikiwa ni pamoja na kutoa usalama kwa waandamanaji. Kipengele cha 37 cha Katiba kinatambua maandamano kama haki ya kimsingi. Kinanukuu, "Kila mtu ana haki, kwa amani na pasipo na silaha, kukusanyika, kuandamana, kuteta, na kuwasilisha maombi kwa viongozi wa umma.

Haki hii inaweza kuainishwa katika kipengele cha 24 (3) ikishirikiana na Kipengele cha 24 (1),[26] au ikiwa tangazo la mkutano mwingine katika ukumbi huo huo, wakati, na tarehe tayari zimepokelewa.[27] Pia inadhibitiwa chini ya Sheria ya Agizo la Umma (Public Order Act), ambayo inasema kwamba kusanyiko linaweza kusitishwa au kuzuiliwa wakati kuna uwazi, sasa, au hatari inayowezekana ya kukiuka kwa amani au utaratibu wa umma. Mkusanyiko ulio wa amani pia unalindwa chini ya sheria za kimataifa, na vizuizi vinaweza kuwekwa "kwa maslahi ya usalama wa kitaifa au usalama wa umma, utaratibu wa umma, ulinzi wa afya ya umma au maadili au ulinzi wa haki na uhuru wa wengine."[28]

Kikundi cha Social Justice Centres Working Group, pamoja na asasi za kiraia (civil society) nchini Kenya, mara kwa mara hubaini kutotii sheria kwa polisi na matumizi ya nguvu kupindukia katika usimamizi wa maandamano. Kutotii huku ni licha ya mamlaka kupokea agizo,[29] kama ilivyoainishwa na sheria ya Kenya, ya mpango wa mkutano uliokusudiwa wa watu 3 na zaidi ya siku 14 kabla ya kufanyika.[30] Vijana walioshiriki walisema kwa uwazi kuwa polisi huamua kwa haraka kutumia risasi za moja kwa moja; kuwapiga waandamanaji kwa viboko, kutumia adhabu ya pamoja kwa watu wote walio katika eneo la maandamano, wakiwemo pia wapita njia; na kutekeleza ukatili wa kijinsia dhidi ya waandamanaji wa kike na wapita njia wanaopatikana kwenye maandamano hayo.[31]

Usimamizi sahihi wa mikusanyiko ya amani hutaka kila mtu anayehusika aheshimu haki za aina nyingi. Haki hizi ni pamoja na uhuru wa kupeana maoni na kujieleza; uhuru wa kushirikiana; uhuru wa mawazo, dhamiri, dini, au imani; haki ya kuishi na uadilifu wa mwili (ambayo ni pamoja na haki ya usalama); haki ya kutodhulumiwa na ukatili, unyama, kubezwa au kuadhibiwa; na haki za mchakato unaofaa, kuendeleza kesi kwa haki, na suluhisho bora kwa ukiukwaji wa haki za binadamu.[32]

Mapendekezo Dhidi Ya Sera za Polisi Katika Vikao Vya Mazungumzo Na Vijana

Polisi wanapaswa kuzingatia katiba na kuheshimu utawala wa sheria na utofauti wa watu wa Kenya kulingana na tabaka, utamaduni, dini, lugha, na kitambulisho cha kijinsia

26 Limitation of Rights and Fundamental Freedoms under Article 24 (1) and (3) reads:
"(1) A right or fundamental freedom in the Bill of Rights shall not be limited except by law, and then only to the extent that the limitation is reasonable and justifiable in an open and democratic society based on human dignity, equality and freedom, taking into account all relevant factors, including
(3) The State or a person seeking to justify a particular limitation shall demonstrate to the court, tribunal or other authority that the requirements of this Article have been satisfied."

27 Section 5(4) Public Order Act.

28 Article 19, Independent Policing Oversight Authority, KNCHR, and United Nations Human Rights Office of the High Commissioner, "The Right to Freedom of Peaceful Assembly: A Checklist for the Kenyan Police and the Public" (2017), 6.

29 Section 5(5) Public Order Act.

30 Section 5(2) Public Order Act.

31 KNCHR, "Mirage at Dusk."

32 Article 19 et al., "The Right to Freedom of Peaceful Assembly." The National Police Service and the state should understand that in the long term, this approach to policing tends not only to harden criminals but also to undermine good policing efforts undertaken by other police officers. As a young member of the Dandora Social Justice Centre explained, "Collective punishment of youth through swoops conducted in slums have ended up being counterproductive as the youth stay indoors until the swoop hours are over, after which they venture out. In the process, some engage in crime without fear of arrest as officers leave after collecting bribes."

wakati wa kutoa usalama kwa wote, haswa vijana. Ripoti ya Ransley inadokeza baadhi ya maadili na kanuni muhimu ambazo mashirika ya polisi lazima viziheshimu na kutii, ikiwa ni pamoja na kutambua na kuheshimu, thamani na uadilifu wa kila Mkenya, kujitolea kwa matumizi ya nguvu inayofaa na matumizi ya nguvu kupidukia wakati tu afisa wa polisi au mtu mwingine yuko katika hatari ya kufa au kujeruhiwa mwilini, kuwahakikishia watu wote (bila kujali kabila, dini, jinsia, au ulemavu) ya ulinzi sawa chini ya sheria, na usikivu wa malalamiko ya raia.

Mapendekezo mwafaka ambayo yametokana na mazungumzo na vijana juu ya tamaduni za ulinzi wa polisi nchini Kenya ni pamoja na yafuatazo:

- Jumuiya ya Building Bridges Initiative (BBI) to Unity Advisory inafaa kukuza ushirikishwaji kwa kualika Kikundi cha Social Justice Centres Working Group kuwasilisha mswada kuhusu uzoefu wao na kushirikiana katika kutoa maoni kwa serikali kuhusu mageuzi au mabadiliko ya sekta ya usalama, ikisisitiza ulinzi wa haki za binadamu kama lengo la kimsingi na kuhakikisha kuwa malalamiko ya vijana kuhusiana na polisi yanashughulikiwa ipasavyo.

- Ili kuzuia ukiukaji wa siku za usoni na kukuza uwazi na heshima ya haki za kibinadamu, mapendekezo ya hili Jumuiya yanapaswa kujumuisha hatua za uwajibikaji kwa ukiukwaji wa zamani uliofanywa na maafisa wa polisi na maafisa wengine wa sekta ya usalama. Mapendekezo haya yanapaswa kujumuisha mapendekezo muhimu ya mageuzi ya sekta ya usalama kutoka kwa ripoti za michakato ya kitaifa za hapo awali — TJRC, Tume ya Uchunguzi ya Vurugu za baada ya Uchaguzi (CIPEV), na Ransley — Ikiwemo pia kutoka kwa Wakala wa Independent Policing Oversight Authority (IPOA).

- Mawakala wa uangalizi, kama vile IPOA, KNCHR, na Kitengo cha Masuala ya Ndani (Internal Affairs Unit), wanapaswa kuunda ushirika thabiti na Social Justice Centres Working Group kwa lengo la kuboresha kiwango cha ulinzi wa polisi katika mitaa ya mabanda na ule wa vijana.

Serikali inapaswa kuunga mkono wazo la Jamii la Social Justice Centres Working Group la kuunda makumbusho ya vijana ambao wameathirishwa na sekta ya usalama kupitia vifo vya jinai, kutokomea kwa ghafla, pamoja na wale wa asili ya Kisomali-Kenya ambao ndio wameathiriwa zaidi na ukiukwaji unaotokana na vita vya serikali dhidi ya ugaidi na misimamo mikali na yenye vurugu ya kidini.

Hitimisho

Kama ilivyoangaziwa wazi na Rais Kenyatta na Mheshimiwa Odinga katika uwasiliano wao wa pamoja, kuhakikisha kuhusishwa na kumaliza utengwaji ni mojawapo ya changamoto kubwa ambayo iwanakabili Wakenya. Vijana, na sio wale tu wanaoishi katika mitaa ya mabanda ya mijini, wameendelea kulalamika kwa kujihi wametengwa katika nyanja zote, ikiwemo na kutokana na mwenendo wa maafisa wa sekta ya usalama. Kwa kweli, michakato ya zamani iliyoanzishwa na serikali (ikiwemo, miongoni mwa nyingine, ripoti ya TJRC, ripoti ya CIPEV, na mchakato wa BBI) zimezungumzia masuala yanayohusiana na wanawake na wasichana, wanaume na wavulana, na jamii zenye uwakilishi mdogo, lakini hawajashughulika haswa na vijana kama kundi, licha ya takwimu kuonyesha kuwa wao huunda asilimia kubwa ya idadi ya watu. Sekta ya usalama ni muhimu katika kulinda ujumuishaji, haswa kwa vijana.

ictj chapisho fupi

Mabadiliko Katika Sekta Ya Usalama Ya Kenya

Tamaduni na mazoea ya sekta ya usalama lazima zirekebishwe ili haki za binadamu ziheshimiwe na kulindwa kulingana na sheria za kitaifa na sheria za kimataifa za haki za binadamu. Kwa hivyo, ustawi wa maafisa wa sekta ya usalama (maafisa wa polisi na wengine) lazima ushughulikiwe pia.

Mchakato wa kujenga Kenya yenye mshikamano thabiti utafanikiwa ikiwa kuna ujumuishaji kwa wote. Kwa kawaida, maafisa wa sekta ya usalama, hususana maafisa wa polisi, wataegemea kuheshimu haki za binadamu ikiwa haki zao wenyewe pia zinaheshimiwa. Mazingira ya kazi kwa maafisa wa polisi hayapaswi kuwa ya kusikitisha na kutishia; mazingira yao ya kazi yanapaswa kuwa ya kuwaunga mkono na ya kitaalam ambayo yanaheshimu haki za maafisa hawa.

ictj chapisho fupi

Mabadiliko Katika Sekta Ya
Usalama Ya Kenya

ICTJ Justice Truth Dignity

The International Center for Transitional Justice works across society and borders to challenge the causes and address the consequences of massive human rights violations. We affirm victims' dignity, fight impunity, and promote responsive institutions in societies emerging from repressive rule or armed conflict as well as in established democracies where historical injustices or systemic abuse remain unresolved. For more information, visit **www.ictj.org**

ICTJ Kenya
Mtito Andei Apts. House No. C1
Mtito Andei Road
Nairobi, Kenya
Tel: +254 725 000958